# BWANA YESU ALIPOKWISHA KULA

**Wimbo wa Komunyo**
**Alhamis Kuu**

Fr. G. Kayetta




1. Bwana Yesu alipokwisha kula pamoja na wafuasi wake/ Aliwaosha miguu.
2. Akawaambia mwafahamu niliyowatendea/ Mimi niliye Bwana na mwalimu wenu.
3. Nimewapa mfano/ Ili mtende nanyi vile vile.
4. Amin, amin nawaambia ninyi/ Mtumwa si mkuu kuliko Bwana wake.
5. Wala mtume si mkuu/ Kuliko yeye aliye mpeleka.
6. Mkiyajua hayo/ Heri ninyi mkiyatenda.
7. Amin, amin nawaambieni/ Yeye ampokeaye mtu fulani yeyote nimpelekaye anipokea mimi.
8. Naye anipokeaye mimi/ Ampokea yeye aliyenipeleka.
9. Kisha Yesu akasema amri mpya nawapeni/ Amri mpya mpendane.
10. Kama vile nilivyowapenda ninyi/ Nanyi mpendane vivyo hivyo.
11. Hivyo watu wote watambue kuwa ninyi wanafunzi wangu/ Mkiwa mnapendana ninyi kwa ninyi.